**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Simu +255 22 211 3165
Nukushi: +255 22 212 4576
Barua pepe: cl@ardhi.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:

1 MTAA WA ARDHI,
S.L.P. 9132,
11477 DAR ES SALAAM,

**Kumb. Na. LD/PW/12805/17** **03/01/2023**

Mkurugenzi Mkuu,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania, (TIC)
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM

TANZANIA INVESTMENT CENTRE
RECEIVED
03 JAN 2023
P. O. Box 938
DAR-ES-SALAAM

**Yah: KUTANGAZA NA KUMILIKISHA VIWANJA NA. 1, 2, 3, 5, 6 & 7 KITALU "D"ENEO LA MBEZI, HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA, KWA AJILI YA UWEKEZAJI**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

2. Tumepokea maombi ya kumilikisha viwanja tajwa hapo juu kwa ajili ya uwekezaji kwa maslahi ya Kampuni ya **KEDA (TANZANIA) CERAMICS CO LTD** yenye cheti cha usajili **(Certificate of Incentives no.202211973).**

3. Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizowasilishwa Kampuni hii ilipata ardhi hiyo kwa njia ya mauziano toka kwa wamiliki wa asili na kujigaramia upangaji na upimaji. Baada ya taratibu za upangaji na upimaji kukamilika, kampuni kupitia Halmashauri imewasilisha maombi ili iweze kumilikishwa kupitia kituo chako kwa kuzingatia fungu la 19(2) (b) la sheria ya Ardhi sura 113 toleo la mwaka 2019.

4. Kwa kuzingatia ufafanuzi huo, tumeandaa **Land Form no 1** ambayo tayari imesainiwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Pwani kwa ajili ya kuitangaza ardhi hii kuwa ya uwekezaji na inawasilishwa kwako.

5. Pamoja na barua hii, fomu husika kwa kila kiwanja kulingana na matumizi zimeambatishwa kwa hatua zako na kisha kuiwasilisha kwa ajili ya kutangazwa.

Tunategemea ushirikiano wako.

Bishanga, T.H
**K.n.y: KAMISHNA WA ARDHI MSAIDIZI**
**MKOA WA PWANI.**

**Nakala:** Keda (Tanzania) Ceramics Co Ltd
S. L. P 61701,
**DAR ES SALAAM.** (Kwa taarifa)